**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# CHUO CHA UALIMU MANDAKA

# KANUNI, TARATIBU NA SHERIA ZA CHUO

## TOLEO LA 2023

## 1.0 Utangulizi

Sheria hizi ni mwongozo wa namna ya kuishi na kuenenda kwa Wanachuo wote wa Chuo cha Ualimu Mandaka wawapo Chuoni na nje ya Chuo. Sheria hizi zinalenga kudumisha nidhamu na kujenga uhusiano mzuri baina ya mwanachuo na Jamii nzima ya Chuo cha Ualimu Mandaka pamoja na mazingira yanayozunguka Chuo. Hivyo, ni lazima kwa mujibu wa Sheria za Chuo kila Mwanachauo kupata nakala ya sheria za Chuo. Aidha, Mwanachuo anapaswa kuweka saini na kuirudisha nakala iliyosainiwa kwa Mwadili wa Wanachuo.

## 2.0 Utii na Heshima

a. Mwanachuo anapaswa kutii sheria za Nchi, Sheria za Chuo na mamlaka zote zilizopo. Aheshimu Alama za Taifa zikiwemo Wimbo wa Taifa, Bendera ya Taifa, n.k. Aidha, ni kosa kwa mwanachuo kukosa utii na heshima kwa jamii yote ya chuo.

b. Mwanachuo anapaswa ajiheshimu na afuate sheria zote kwa mujibu wa taratibu za Chuo.

*Mwanachuo atakayefanya kosa la kutotii sheria za nchi au sheria za chuo ataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria aliyoivunja.*

*Mwanachuo akithibitika amevunja sheria hii, atapewa onyo kwa maandishi, kufanya kazi za nje ya darasa, au kusimamishwa masomo kwa siku zisizozidi kumi na nne (14) au adhabu zote kwa pamoja.*

## 3.0 Ruhusa kwa Mwanachuo

a. Ni kosa kwa mwanachuo kutoka nje ya chuo bila ruhusa ya maandishi. Ruhusa kwa Mwanachuo yeyote kwenda nje ya Chuo muda wa masomo (muda wa mchana) zitatolewa na Mkufunzi wa zamu. Aidha, ruhusa zote za kulala nje ya Chuo zitatolewa na Mkuu wa Chuo.

b. Ni kosa kwa mwanachuo kuongeza muda wa ruhusa bila kibali cha mamlaka iliyompa ruhusa.

*Mwanachuo atakayethibitika kufanya kosa hili au kuchelewa kurudi Chuoni atapewa adhabu itakayopangwa ikiwa ni pamoja na onyo au kusimamishwa masomo kwa muda usiozidi siku kumi na nne (14).*

*Aidha kwa Mwanachuo yeyote atakayeondoka Chuoni bila ruhusa kwa muda wa wiki moja na kuendelea bila ruhusa atasimamishwa masomo kwa muda usiozidi siku ishirini na moja (21) ikiwa atakuwa kwa siku 90 kulingana na sheria ya utoro atafukuzwa chuo.*

c. Mwanachuo yeyote aliyesimamishwa chuo akikukutwa katika mazingira ya Chuo bila kibali cha maandishi juu ya uwepo wake kutoka uongozi wa Chuo wakati angali akitumikia adhabu ya kusimamishwa Chuo kwa muda ikiwa haijakoma atakuwa ametenda kosa

*Mwanachuo wa aina hii atapewa onyo kwa maandishi, adhabu za ndani na adhabu ya kusimamishwa itaanza upya au adhabu zote kwa pamoja.*

## 4.0 *Bidii katika Masomo (Taaluma)*

Chuo ni taasisi ya kitaaluma ambapo kila mwanachuo anapaswa kutambua kuwa amejiunga na chuo kwa nia ya kusoma kwa bidii na kuwa na ufaulu wa kiwango cha juu. Hivyo, itakuwa:

a. Ni kosa kwa mwanachuo kutohudhuria vipindi darasani au muda wa mtwalaa (Prepo) au shughuli zingine za kitaaluma chuoni.

b. Ni kosa kwa mwanachuo kutoonesha bidii katika masomo na kutoonesha maendeleo ya ufaulu wa kitaaluma. Aidha, mwanachuo hapaswi kupata gredi ‘F’ katika masomo yake.

c. Ni kosa kwa mwanachuo kutofanya mazoezi, majaribio na mitihani iliyotolewa na Mkufunzi husika au chuo au kanda.

d. Ni kosa kwa mwanachuo kufanya udanganyifu kwenye mazoezi, majaribio na mitihani.

*Mwanachuo atakayebainika kwa makosa haya atapewa adhabu za ndani au atasimamishwa masomo kwa muda wa siku zisizozidi kumi na nne (14) au kutakiwa kuahirisha/kurudia mwaka wa masomo au kusimamishwa mafunzo au adhabu zote kwa pamoja.*

## 5.0 Ulevi

a. Ni kosa kwa mwanachuo kulewa kwa muda wote wa mafunzo.

b. Ni kosa kwa mwanachuo kutumia au kuuza madawa ya kulevya kama vile bangi, mirungi, n.k na vitu vyote vinavyoendana na hivyo akiwa ndani au nje ya mazingira ya Chuo.

c. Ni kosa kwa Mwanachuo kuhifadhi kilevi cha aina yoyote katika mazingira ya chuo.

*Mwanachuo atakaye thibitika kutenda kosa namba 4 (b) kupelekwa polisi na atafukuzwa Chuo. Mwanachuo akifanya kosa 4 (a & c) atapewa onyo kwa barua, adhabu kali,*

*kusimamishwa Chuo kwa muda wa siku zisizozidi kumi na nne (14) au vyote kwa pamoja na asipobadilika basi mwanachuo huyo atakosa sifa ya kuendelea na masomo na atafutiwa usajili rasmi.*

## 6.0 Umiliki wa Silaha

a. Ni kosa kwa Mwanachuo kumiliki au kushikilia silaha zinazoweza kuhatarisha usalama au amani ya wanajumuiya ya Chuo cha Ualimu Mandaka kama vile silaha za moto, kemikali hatarishi na vifaa vyenye ncha kali.

*Mwanachuo atayekutwa na kosa hilo ataadhibiwa kwa onyo, kupata adhabu ya ndani itakayopangwa au kufukuzwa bwenini au kupelekwa polisi na kuachishwa mafunzo au vyote kwa pamoja kutegemeana na aina ya silaha aliyojihusisha.*

## 7.0 Mavazi na Unadhifu

a. Mwanachuo atatakiwa kuvaa mavazi yenye heshima, safi na nadhifu kulingana na sheria ya mavazi ya mtumishi wa umma na ya Chuo cha Ualimu Mandaka.

b. Sare au mavazi rasmi ya Chuo yatavaliwa wakati wote wa vipindi au mwanachuo anapotoka nje ya Chuo. Aidha, mwanachuo atapaswa kuzingatia yafuatayo:

i. Sketi kwa wanachuo wa kike (isiyobana) itapaswa kuwa na ‘V’ na si pungufu ya inchi 5 kuanzia kwenye magoti kushuka chini. Aidha, Suruali isiyobana kwa wanachuo wa kiume yenye upana wa chini inchi 14.

ii. Siku ya ijumaa wanachuo wataruhusiwa kuvaa tisheti rasmi ya chuo wakati wa masomo. Vilele, mwanachuo atapaswa kuvaa viatu vyeusi vifupi, soksi nyeusi kwa wavulana na soksi nyeupe kwa wasichana

iii. Ni kosa kwa mwanachuo kuvaa kaptula, nguo zenye picha au michoro ya ajabu, malapa, nguo za mipasuo inayovuka magoti, suruali za kubana, sketi fupi na za kubana au kofia katika maeneo ya Chuo

iv. Aidha, ni kosa kuvaa mapambo, kupaka wanja, hina na rangi za midomo au kucha wakati wa masomo.

*Mwanachuo atakayebainika kukiuka sheria hii, atajazishwa fomu ya onyo kali au adhabu za ndani au kusimamishwa masomo kwa muda usiozidi siku 14. Au vyote kwa pamoja.*

**8.0 Unyanyasaji wa kijinsia au wa namna nyingine**

Unyanyasaji wa kijinsia au wa kimaumbile au wa aina yoyote haukubaliki. Hii ni pamoja na;

a. Kumlazimisha mtu kwa kumtaka kimapenzi kwa kutumia maneno, ishara, picha au vitisho vyenye maudhui ya kimapenzi au kumsababishia mtu kukosa amani ama kushindwa kutekeleza majukumu yake.

b. Kutumia ishara za kufanya mapenzi katika mazingira ya Chuo au kumshikashika mtu bila ridhaa yake.

c. Kumkashifu au kumnyanyapaa mtu yeyote kutokana na maumbile aliyonayo au hali alionayo.

*Kwa Mwanachuo atakayebainika kuwa na kosa hilo la unyanyasaji atapewa adhabu za ndani zitakazopangwa au atasimamishwa masomo kwa muda usiozidi siku ishirini na moja (21) au adhabu zote kwa pamoja.*

**9.0 Wizi wa mali ya Umma au binafsi**

a. Ni kosa kwa mwanachuo yeyote kujihusisha na vitendo vya wizi kwa namna yoyote.

b. Ni kosa kwa mwanachuo kushirikiana na mtu au mwanachuo mwingine kujihusisha na wizi au kununua vitu vilivyoibwa kwa mtu mwingine. Aidha, kujihusisha na wizi wa kimtandao au utapeli.

*Adhabu yake ni kusimamishwa masomo kwa muda usiozidi siku 21, kulipa au kufidia mali iliyoibwa, kufukuzwa bwenini, kupelekwa polisi au vyote kwa pamoja.*

**10.0 Ugomvi**

a. Ni kosa kwa mwanachuo kupigana na mwanachuo mwezake au raia yeyote.

b. Ni kosa kwa mwanachuo kuanzisha, kujihusisha, kusababisha au kuchochea ugomvi ndani au nje ya mazingira ya Chuo.

c. Mwanachuo atakayefanya vitendo vyovyote vitakavyopelekea ugomvi au kumdhuru mtu na mali yake katika mazingira ya Chuo, hii ni kwa Mwanachuo dhidi ya Mwanachuo mwenzake, mfanyakazi na mwanajumuiya ya Chuo cha Ualimu Mandaka au nje ya Chuo atakuwa amevunja sheria hii.

*Mwanachuo atakayebainika kuwa ameshiriki kuvunja sheria hii atasimamishwa masomo kwa muda usiozidi siku ishirini na moja (21), kulipa/kufidia vitu vilivyoharibiwa, kufukuzwa bwenini, kupelekwa polisi au kufukuzwa chuo.*

**11.0 Ubakaji, ulawiti na usagaji/ushoga**

a. Ni kosa la jinai kwa mwanachuo kujihusisha na ubakaji, ulawiti, usagaji/ushoga chuoni au mahali popote nchini. Aidha, ni kosa kwa wanachuo wawili wa jinsia moja au tofauti kulala kitanda kimoja.

*Mwanachuo atakeyebainika kujihusisha na vitendo hivyo atasimamishwa mafunzo, kupelekwa polisi na kufukuzwa Chuo au kutumikia adhabu zote mbili kwa pamoja.*

**12.0 Kukataa wito/kugoma au kushawishi mgomo**

a. Ni kosa kwa mwanachuo kukataa kuhudhuria vikao au mikutano halali iliyoitishwa na uongozi wa Chuo. Aidha, kila mwanachuo anapaswa kushiriki kazi zote zikiwepo usafi binafsi, usafi wa mazingira, uzalishaji mali, michezo na shughuli za kitaifa zitakazo elekezwa na uongozi wa Chuo.

b. Ni kosa kwa mwanachuo kukataa/kugomea wito au adhabu halali.

c. Ni kosa kushawishi au kujenga mazingira mbalimbali ya ushawishi wanachuo wengine kushiriki kukataa wito/kugoma.

*Mwanachuo atakayekutwa na kosa hili atapewa barua ya onyo, adhabu ya ndani ya chuo ikiwemo kusimamishwa masomo kwa kipindi kisichozidi siku 21 au adhabu zote pamoja*

**13.0 Matumizi ya Mali ya Umma na Miundombinu ya Chuo**

a. Ni kosa kuhamisha samani za Chuo cha Ualimu Mandaka kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine bila ya kibali.

b. Ni kosa kwa mwanachuo kupoteza au kuharibu kifaa/mali ya chuo kwa uzembe au kwa kukusudia.

c. Ni kosa kwa mwanachuo kupeleka chakula bwenini. Chakula chote kitaliwa bwaloni au Kantini.

d. Ni kosa kwa mwanachuo kuhatarisha usalama wa mali za chuo na wanachuo wenzake

e. Ni kosa kufanya matumizi mabaya na hatarishi ya mifumo ya umeme, maji, TEHAMA, nk. ndani ya chuo. Ikiwa ni pamoja na kuunganisha nyaya za umeme kinyume na mfumo uliowekwa katika jengo husika, matumizi ya mishumaa, hita, jiko au birika za umeme, vifaa vya kukaushia nywele (drier), blanketi za umeme na uharibifu wa miundombinu ya maji, kuchafua kuta za jengo au kupita sehemu isiyo rasmi ndani ya chuo.

*Mwanachuo atakayetenda makosa haya atajazishwa fomu ya onyo au karipio na kupewa adhabu ya ndani, kulipa au kugharamia matengenezo ya hasara/uharibifu/madhara aliyosababisha, kufukuzwa bwenini, kusimamishwa mafunzo siku zisizozidi ishirini na moja (21), kufukuzwa chuo au adhabu zote kwa pamoja.*

## 14.0 Matumizi ya Lugha yasiyofaa

a. Ni kosa kwa mwanachuo kutumia lugha ya matusi, kejeli au ya vitisho kwa mwanajumuiya yeyote wa Chuo au raia.

b. Hairuhusiwi kwa Mwanachuo kuandika au kuchora picha zinazoashiria matusi, kejeli, kashfa au udhalilishaji ndani na nje ya chuo cha Ualimu Mandaka.

*Mwanachuo yeyoye atakayefanya kosa hili chini ya sheria hii atasimamishwa masomo kwa kipindi kisichozidi siku ishirini na moja (21) na akirudi atatumikia adhabu za nje kadri zitakavyoamuliwa.*

## 15.0 Mawasiliano chuoni

a. Ni kosa kwa mwanachuo kutumia mitandao ya kijamii vibaya kwa kuandika, kurekodi au kunakili machapisho yenye maudhui yasiyofaa na kuyarusha mitandaoni kinyume cha sheria, kanuni na taratibu za nchi au Chuo.

b. Ni kosa kwa mwanachuo kutoa taarifa zozote za Chuo kwa mtu yeyote bila kuruhusiwa na uongozi wa Chuo. Aidha, taarifa zote zitatolewa na uongozi wa chuo kwa mzazi/mlezi.

c. Ni kosa kutumia simu muda wa vipindi, mitihani, muda wa prepo au wakati wa kazi rasmi zikiwemo za uzalishaji mali.

*Mwanachuo atakayebainika kuvunja sheria hii atanyang'anywa simu muhula mzima au atasimamishwa mafunzo kwa muda wa siku zisizozidi ishirini na moja (21), kupelekwa polisi au kufukuzwa Chuo au adhabu zote kwa pamoja.*

## 16.0 Mahusiano Chuoni

a. Ni kosa kwa mwanachuo yeyote kuonyesha dalili kwa namna yoyote kuwa na mahusiano ya kimapenzi/kuishi kama mke na mume na mwanachuo mwenzake au mfanyakazi wa chuo au mtu mwingine yeyote.
b. Hairuhusiwi kwa mwanachuo kuwa na Ujauzito muda wote wa Mafunzo. Aidha, ni kosa la jinai kutoa Ujauzito.

i. *Mwanachuo atakayebainika* kuwa na mahusiano ya kimapenzi ama ya kuishi kama mke na mume *atasimamishwa masomo kwa muda wa siku zisizozidi 21.*

ii. *Na endapo mwanachuo atabainika kuwa na ujauzito na aliyesababisha ni mwanachuo mwenzake, wote wawili watalazimika kuahirisha mwaka wa mafunzo.*

iii. *Endapo mwanachuo atabainika kuwa ametoa ujauzito atafukuzwa Chuo na kupelekwa polisi ili kuruhusu sheria za nchi kuchukua mkondo wake.*

## 17.0 Wageni na Kutembeleana

a. Ni kosa kwa mwanachuo wa jinsi ya kike kuingia mabweni ya wavulana. Aidha, ni kosa pia kwa mwanachuo wa jinsi ya kiume kuingia kwenye mabweni ya wasichana.

b. Ni kosa kwa mwanachuo kumkaribisha mgeni ndani ya chuo bila kutoa taarifa kwa Mkufunzi wa zamu na kumruhusu kuingia ndani ya chuo.

c. Ni kosa kwa mwanachuo kumpeleka au kumkaribisha mgeni bwenini.

d. Mwanachuo haruhusiwi kwenda nyumba ya Mtumishi wa chuo bila kibali cha Mwadili.

*Mwanachuo atakayethibitika kutenda kosa hili atapewa adhabu za kkazi za ndani, kusimamishwa masomo kwa kipindi kisichozidi siku kumi na nne (14) au adhabu zote mbili kwa pamoja.*

***NB: Kila adhabu inayohusisha kurudishwa nyumbani, mwanachuo akirudi atapaswa kuwa na mzazi/mlezi na atatakiwa kulipa madeni yote kama anadaiwa. Pia, atafanya kazi za nje kukamilisha adhabu kulingana na uzito wa kosa lake.***

## 18.0 Ahadi ya Utii wa Sheria

Mimi:_______________________________________Mchepuo_________Darasa_________ nimezisoma sheria za Chuo cha Ualimu Mandaka na kuzielewa. Naahidi kuziishi na kuzifuata kikamilifu muda wote wa Mafunzo ya Ualimu hapa Chuoni.

Saini: ____________________________ Tarehe: ____________________

**NB: MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANACHUO KUFUKUZWA CHUO**

i. Wizi.
ii. Uasherati, ubakaji, usagaji na ushoga.
iii. Ulevi, uvutaji wa bangi na matumizi ya madawa ya kulevya.
iv. Makosa yoyote ya jinai.
v. Kupiga au kupigana.
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma /chuo
vii. Kudharau bendera ya Taifa.
viii. Kushiriki au kutoa mimba.
ix. Kugoma, kuchochea mgomo au kuvuruga amani na usalama wa chuoni.
x. Kukataa adhabu kwa makusudi.
xi. Kufanya matendo yanayohatarisha usalama wa chuo na wanajamii na
xii. Kutowajibika kitaaluma.